



THE ANGLICAN CHURCH OF TANZANIA

P. O. Box 899, Dodoma, Tanzania Tel: +255 (0) 262321437/2324574 Fax: +255 (0) 262324565
Email: act@anglican.or.tz **Archbishop:** The Most Rev. Maimbo William Fabian Mndolwa,
General Secretary: The Rev. Can. Mecka Ogunde.

TAARIFA KWA UMMA

1. Sisi Dkt. Maimbo William Mndolwa, Askofu Mkuu wa Kanisa Anglikana Tanzania, kwa niaba ya Maaskofu, Wachungaji na Wakristo wote wa Kanisa Anglikana Tanzania, kwa masikitiko makubwa tunaungana na watazania wenzetu kutoa salamu za pole kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli na familia yote ya Mkapa kwa msiba mkubwa wa Mzee wetu **Benjamin William Mkapa**, Rais mstaafu wa Awamu ya Tatu. Tunamwomba Mungu awe faraja kwa Rais wetu, familia ya marehemu na watazania kwa ujumla.
2. Sisi Kanisa Anglikana Tanzania, tunatambua mchango mkubwa wa Mzee wetu **Mhe. Benjamin William Mkapa**, katika kusaidia maendeleo ya huduma za Kanisa kabla ya kuwa Rais, akiwa Rais na hata baada ya kustaafu kwake. Kipekee tunaenzi huduma yake ya kuwezesha Kanisa Anglikana Tanzania kuwa na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Yohana. Mzee Mkapa alipenda watu wake, alipenda Kanisa na daima alikuwa ni muumini wa kielelezo kwa wengi. Alikuwa mstari wa mbele katika kusaidia masuala mbalimbali yanayohusu madhehebu na imani za watazania.
3. Tunakumbuka wakati mwingi tulipomwomba katika matukio mbalimbali ndani ya Kanisa hakisita kufika na alitusaidia. Moyo wake ulikuwa kama yule Akida wa Kapernamu anayetajwa katika Injili ya Luka Mtakatifu Sura ya 7: 1-10 maana, alilipenda taifa letu, naye alitusaidia katika huduma mbalimbali za kueneza injili.
4. Tukitazama mambo makubwa aliyofanya katika maisha yake, nasi hatuna budi kumtukuza Mungu sana. Tunaiombea familia yake na watazania wote ili Mungu akazidi kuwa faraja kwetu sasa na katika kipindi chote cha msiba huu mzito.

“Yesu akamwambia, Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi; naye kila aishiye na kuniamini hatakuwa kabisa hata milele” (Yohana 11:25-26)

5. Roho yake **Mhe. Benjamin William Mkapa**, na Roho za Marehemu wote walioitwa katika Bwana, wapumzike kwa Amani,

AMIN



The Most. Rev. Dr. Maimbo William Fabian Mndolwa, Tanzania na Tanga

ASKOFU MKUU WA KANISA ANGLIKANA TANZANIA

24 Julai, 2020